MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Maadhimisho ya Siku kuu ya Kiswahili Duniani: Upi mwelekeo mwafaka?

Frida Miruka[a*], Ernest Mohochi[b], Pamela Ngugi[c], Juliet Jagero[d]

[a]*Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi, Shule ya Elimu, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kakamega, Kenya*

[b]*Chuo Kikuu cha Kibabii, Bungoma, Kenya*

[c]*Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Kenya*

[d]*Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga, Kenya*

## IKISIRI

Lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Kiafrika zinazozungumzwa zaidi ulimwenguni ikiwa na zaidi ya wasemaji Millioni 250. Hali hii pamoja na hadhi na dhima ya Kiswahili katika jamii mbalimbali ilipelekea shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) katika kikao chake cha 41 kutangaza Julai tarehe 7 kuwa siku kuu ya Kiswahili duniani. Hatua hii ilikifanya Kiswahili kuwa lugha ya kwanza ya Kiafrika kutambuliwa na Umoja wa Mataifa na kuwa na siku maalum ya kuadhimishwa. Katika maadhimisho ya tatu yaliyofanyika mwaka 2024 kote duniani, Jumuia ya Afrika mashariki kupitia Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA) iliandaa sherehe nchini Kenya kwa kushirikiana na Wizara ya Jinsia, Utamaduni, Sanaa na Turathi. Wadau waliohusishwa walikuwa baadhi ya wanataaluma, wapenzi wa lugha ya Kiswahili na Jamii ya Waswahili mjini Mombasa. Maadhimisho haya hata hivyo hayakuwahusisha wadau wote ambao wamechangia kuiinua lugha hii na kuipa sura ya Lugha ya Ulimwengu. Baadhi yao ni wataalamu kutoka vyuo vikuu mbalimbali, waandishi wa vitabu, wanahabari na walimu wa Kiswahili. Mipango ya kuandaa sherehe katika baadhi ya vyuo maalumu haikufua dafu huku vyuo vingine vikiadhimisha siku hii kando na sherehe iliyoandaliwa na KAKAMA. Kukifungia Kiswahili katika jamii na utamaduni wa Waswahili pia kunaishusha hadhi lugha hii kama lugha ya Ulimwengu. Swali linalozuka ni Je, pana haja ya kuweka mpango mwafaka wa kuadhimisha siku hii? Makala hii inaangazia nafasi ya Kiswahili katika jamii na kutathmini Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili kwa lengo la kupendekeza mikakati ya kuyaimarisha ili kujenga taswira ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya ulimwengu. Pendekezo kuu la Makala hii ni kuhimiza ushirikiano wa wadau wote katika maadhimisho ya Siku kuu ya Kiswahili duniani.

## KUHUSU MAKALA

*Maneno Muhimu:*
Nyimbo,
Kiswahili,
Utamaduni,
Siku kuu ya Kiswahili,
Lugha ya Kimataifa,
Ushirikiano

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 12 Mei 2024
Tarehe ya Kurekebishwa: 23 Julai 2024
Tarehe ya Kukubalika: 30 Septemba 2024
Mtandaoni: 27 Novemba 2024

## 1. Utangulizi

Lengo la kuwa na maadhimisho yoyote yale huwa kuifahamisha, kuchachawisha na kuhamasisha jamii kuhusu suala maalum katika jamii husika na ulimwengu kwa jumla. Shirika la Umoja wa Mataifa likishirikiana na mashirika mengine limejitwika jukumu la kutenga siku maalumu pamoja na kuandaa maadhimisho yanayolenga mada tofauti kuhusu maisha ya wanajamii. Kipengele cha lugha ni miongoni mwa masuala yanayopigiwa upato na shirika la Umoja wa Mataifa. Baadhi ya lugha ambazo zinaadhimishwa kwa siku maalumu ni Kiarabu (tarehe18, Desemba), Kichina (tarehe 20, Aprili), Kiingereza (tarehe 23, Aprili), Kifaransa (tarehe 20, Machi) Kirusi (tarehe 6, Juni) na Kihispaniola (tarehe 23, Aprili). Lugha ya Kiswahili ndiyo lugha pekee ya kutoka Afrika iliyotengewa siku maalum (tarehe 7 Julai).

Historia ya kutambuliwa kwa lugha ya Kiswahili kimataifa ilianza mnamo mwaka wa 1950 wakati shirika la Umoja wa Mataifa lilipoanzisha kitengo maalumu cha lugha ya Kiswahili chini ya United Nations Radio. Hatua hii ilikifanya Kiswahili kuwa lugha ya kipekee ya Kiafrika katika Kurugenzi la Global Communication of United Nations. Isitoshe, mwanzoni mwa miaka ya 1960, wakati ambamo nchi nyingi za Afrika zilikuwa katika harakati za kujikomboa dhidi ya ukoloni, waandishi na wataalamu wa Kiswahili kama vile Wole Soyinka walianza kutoa wito wa matumizi ya Kiswahili kama lugha ya Bara la Afrika, (Chimerah, 1998). Hali hii pamoja na hadhi na dhima ya

* Mwandishi Mkuu. Simu: +254727247403; Barua Pepe: fmiruka@mmust.ac.ke
Mhariri: Benard Okal, Chuo Kikuu cha Maseno, Kenya.
Nukuu: Frida M., Ernest M., Pamela N., & Juliet J. (2024). Maadhimisho ya siku kuu ya kiswahili duniani: Upi mwelekeo mwafaka? Jarida la Kiswahili Sanifu 1(2024), 33 – 40.

© 2024 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

Kiswahili katika nchi mbalimbali ilipelekea shirika la Umoja wa Mataifa UNESCO katika kikao chake cha 41 kutangaza Julai tarehe 7 kuwa Siku Kuu ya Kiswahili duniani mwaka wa 2021 (UNESCO, 2021).

Kiswahili ni lugha inayozungumzwa na takribani watu Millioni 250 katika nchi 15 zilizo Afrika Mashariki na kwingineko na ni miongoni mwa lugha kumi maalum zinazotambulika ulimwenguni. Lugha hii haitumiki tu kama chombo cha mawasiliano bali pia ni ishara ya umoja, pamoja na utambulisho wa Waafrika wanaoizungumza hii. Kufikia sasa, Kiswahili ni lugha inayotumika katika nchi mbalimbali za Afrika kwa sababu mbalimbali. Kutokana na kusambaa kwake, lugha hii imekubalika katika sehemu nyingi kutekeleza majukumu ya kuwa lugha ya mawasiliano ya kijamii, lugha ya Taifa, lugha Rasmi na lugha ya Kimataifa. Kimsingi, lugha ya Kiswahili imeimarishwa kutokana na michango ya asasi mbalimbali katika jamii husika. Hizi zinajumuisha wizara pamoja na asasi nyingine katika nchi za Afrika na nje ya Afrika. Ni katika muktadha huu ambapo makala hii inatathmini maadhimisho ya Siku Kuu ya Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika mwaka 2024 tangu Kiswahili kupewa siku maalumu kwa lengo la kupendekeza njia mwafaka za kuboresha sherehe za baadaye.

### 1.1. Misingi ya Nadharia

Makala hii imejikita katika nadharia ya Ushirika iliyoasisiwa na Deutsch (1949) na kuendelezwa na Deustsch & Krauss (1962). Wazo kuu la nadharia hii ni kuonyesha matokeo ya ushirikiano, ushindani na ubinafsi katika michakato inayoibua hali hizi katika mashirika. Kwa mujibu wa nadharia hii, utimizaji wa malengo katika hali ya ushirikiano huwa chanya, kwani husaidia wahusika wengine pia kutimiza malengo yao.

Dhana kuu za nadharia hii ni kuwa, hali tatu hubainika katika mashirika mathalan ushirikiano, ushindani na ubinafsi. Katika hali ya ushirikiano, utimizaji wa malengo kwa mshiriki mmoja ni mchakato chanya ambao huwasaidia wengine pia kutimiza malengo yao. Katika hali ya ushindani, malengo ya washiriki huwa na mahusiano hasi ambapo jitihada za kutimiza shabaha za mshiriki mmoja huwa kikwazo kwa wengine. Idara mbalimbali huishia kushindania vifaa na rasilimali za shirika. Ubinafsi, kwa upande mwingine hauhusishi wala kuathiri wengine kwa vyovyote. Deutsch (1949) anadhukuru kuwa ushirikiano humaanisha ukosefu wa mivutano, ushindani na changamoto. Kwamba ushirikiano ndio suluhu kwa changamoto za shirika. Anaeleza kuwa matokeo ya ushirikiano ni kupata usaidizi unaotarajiwa; Mawasiliano mwafaka na ushawishi; Ugawaji na utimizaji wa majukumu kikamilifu; Urafiki na kusaidiana. Tafiti mbalimbali zimethibitisha mawazo haya. Kwa mfano, Deutsch, (1949), Deutsch & Krauss, 1962 na Crombag, (1966) wanadai kwamba watu walio kwenye ushirikiano huelewana na huathiriana kimawazo kwa njia mbalimbali. Pili, Ushirikiano huhimiza utafutaji na utoaji wa taarifa kuhusu kazi za shirika (Zander & Wolf, 1964). Isitoshe, watu katika ushirika huwasiliana, husaidiana na hugawana kazi (Deutsh, 1949; Thomas 1957; Zander & Wolf, 1964). Kinyume cha ushirikiano, ushindani husababisha kudidimia kwa malengo, uchokozi, uadui, uzuizi na ukosefu wa ushawishi (Rocha & Rodgers, 1976; Tjosvold, 1983). Kutokana na maoni ya wataalamu hawa, ni wazi kuwa ushirikiano huchangia katika kuyafikia malengo ya kikundi fulani.

## 2. Nafasi ya Kiswahili

Lugha ya Kiswahili ina nafasi muhimu katika jamii kutokana na matumizi yake ya kutekeleza majukumu maalum katika miktadha anuwai. Kiswahili kimeshamiri kama lugha ya kimataifa, lugha ya ulimwengu, barani Afrika, Afrika Mashariki na katika nchi mbalimbali. Uteuzi wa Kiswahili kama moja wapo ya lugha zinazotambuliwa na UNESCO na kutengewa siku maalum duniani unaashiria hadhi mpya ya lugha ya Kiswahili na haja ya kuweka mikakati mwafaka ya kuikuza.

### 2.1. Lugha za Kimataifa


Lugha zinazozungumzwa ulimwenguni hutofautiana kihadhi. Hili huchangiwa na mambo kama vile: idadi ya watumiaji wake; hali ya kiuchumi na kijamii ya watumiaji wake; historia ya lugha hiyo, ikiwa ni pamoja na matumizi yake katika maandishi; matumizi yake katika nyanja muhimu kama elimu, dini, biashara, siasa, vyombo vya habari na kadhalika. Kutokana na hayo, zipo lugha zinazotumika katika mazingira finyu kieneo na zile ambazo zimevuka mipaka na hutumika katika sehemu mbalimbali ulimwenguni. Kufuatia hilo, kuna lugha za kimataifa kwa sababu ya upanuzi wa mawanda ya matumizi yazo. Dhana hii ya lugha ya kimataifa, anavyodai Guitu (2010) ilifafanuliwa mwanzo kabisa na Smith (1976) kwa kuieleza lugha ya kimataifa kama lugha inayotumiwa na watu wa mataifa tofautitofauti kuwasiliana.

Kiingereza ni moja katika lugha hizo. Utandawazi umeieneza hadi kuifanya lingua franca ya ulimwengu kwani ndiyo lugha inayotumika zaidi miongoni mwa wazungumzaji wa lugha mbalimbali. Hata hivyo, idadi ya wanaoizungumza kama lugha ya kwanza imeendelea kuwa ndogo ikilinganishwa na wale wanaoizungumza kama lugha ya pili au tatu. Crystal (2006) anasema kwamba wakati idadi ya kundi la kwanza inaendelea kupungua ile ya kundi la pili inaongezeka. Aidha, kulingana na Dewi (2012) idadi ya wazungumzaji wasio wazawa ni mara tatu ya wale waitumiayo kama lugha ya kwanza. Matumizi ya Kiingereza kama lugha ya kimataifa yamefafanuliwa na Kachru (1985) kwa kubuni kielelezo ambacho kinazigawa nchi zinazotumia Kiingereza katika makundi matatu: nchi za duara ya ndani, za duara ya nje, na za duara inayopanuka. Anaendelea kufafanua kuwa Kiingereza kilienea kutoka kwa nchi za duara ya ndani kwa sababu wazungumzaji wake walihamia maeneo mengine ya kijiografia, na kikaenea katika nchi za duara ya nje kutokana na ukoloni. Katika nchi za duara inayopanuka, Kiingereza kinaendelea kuenea kwa sababu ya mafunzo ya lugha za kigeni. Kiingereza kimeishia kuwa lugha ya ulimwengu kwa kufanywa ama lugha rasmi katika nchi za duara ya nje au kupewa kipaumbele katika nchi za duara inayopanuka (Dewi, 2012). Hata hivyo, Kiingereza siyo lugha ya pekee yenye hadhi ya kimataifa. Zipo nyingine kama vile Kifaransa, Kihispania, Kichina, Kihindi, Kireno na kadhalika. Kiswahili, kama

tutakavyoona baadaye, kina hadhi hiyo ya lugha ya kimataifa kwa sababu ya sifa zake.

### 2.2. Kiswahili kama Lugha ya Kimataifa

Kama hali ilivyo kuhusu Kiingereza, idadi ya wazungumzaji wazawa wa Kiswahili ni ndogo sana ikilinganishwa na wanaoitumia kama lugha ya pili, tatu au zaidi. Aidha, idadi ya hilo kundi la pili inaendelea kuongezeka kila uchao. Wasomi na wapenzi wa Kiswahili nchini Kenya na Tanzania wanashikilia kuwa Kiswahili hakina mpinzani kama lingua franka Afrika Mashariki. Aidha, lugha hii inaenea kwa kasi barani Afrika na kwingineko kiasi cha kuingia kwenye kundi la lugha za kimataifa (Okombo na Muna, 2017). Hata hivyo, Okombo na Muna (2017) wanadai kwamba dai hilo halijatolewa maelezo ya kitaalamu. Wanatumia kielelezo (Tak.1) cha Kachru (1985) cha Viingereza vya Ulimwengu.




**Tak. 1**: Kutokana na Kielelezo cha Braj Kachru- Three Circles Model of World Englishes (Crystal 1997: 54, katika Okombo and Muna 2017: 58).

Duara ya ndani katika Tak.1 ya Kiswahili inajumuisha Tanzania na Kenya. Hata hivyo, anavyosema Chimerah (1998) maendeleo na matumizi ya lugha hii katika duara hii hayafanani. Kimeenea na kupewa nafasi zaidi nchini Tanzania ikilinganishwa na Kenya. Katika duara hii, elimu, vyombo vya habari, muziki, utafiti na uchapishaji ni miongoni mwa mambo yanayoendelea kuikuza lugha hii. Ni maoni ya Okombo na Muna (2017) kwamba katika duara hii, idadi ya wazungumzaji wa Kiswahili imezidi milioni 100. Tunafikiria kwamba kufikia sasa idadi hiyo imeongezeka sana.

Duara ya nje katika Tak.1 inapaswa kujumuisha maeneo ambamo Kiswahili, japo si lugha asilia, kinatumika na idadi kubwa ya watu na kimepewa majukumu muhimu kama vile kuwa lugha rasmi. Isitoshe, Kiswahili kimepata nafasi ya kuwa lugha rasmi katika Umoja wa Mataifa ya Afrika ili kuimarisha umoja wa nchi za Afrika Mashariki. Fauka ya hayo, kingepaswa pia kutumika kama lugha ya kufundishia. Ingawa hayaonyeshi sifa hizo zote kikamilifu, mataifa ya Uganda, Rwanda, Burundi na Kongo yanaweza kuchukuliwa kuwa maeneo ya duara ya nje katika ufafanuzi wa hali ya lugha ya Kiswahili. Isitoshe, sehemu za Msumbiji na Afrika Kusini nazo zimo duarani. Kulingana na Okombo na Muna (2017) wazungumzaji wa Kiswahili katika duara hiyo ya nje ni takribani milioni 54. Nchi nyingine ni Malawi, Komoro, Madagaska, na kusini mwa Somalia na Sudan ya kusini. Ingawa lugha hii haitumiki kama lugha ya kufundishia katika nchi hizi, ina nafasi kubwa kama somo katika viwango mbalimbali vya elimu katika nchi kama vile Uganda, Rwanda na Burundi. Kwa ujumla, matumizi ya Kiswahili katika duara hii ya nje ni muhimu sana katika kuendeleza hadhi yake kama lugha ya kimataifa.

Hakuna data ya kuonyesha idadi ya wazungumzaji wa Kiswahili katika duara inayopanuka. Hata hivyo, inafahamika kuwa lugha hii inafundishwa katika vyuo vikuu vingi Uropa na Marekani. Kwa mujibu wa Chimerah (1988), na Mutiso (2016) zaidi ya vyuo 100 hufundisha Kiswahili nchini Marekani. Japo si rahisi kutaja idadi kamili ya wanaosoma Kiswahili ughaibuni, Mulokozi (2004) anadai kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya Kiafrika inayofundishwa zaidi ulimwenguni. Wanavyohitimisha Okombo na Muna (2017), Kiswahili kinaendana vizuri na kielelezo cha Kachru. Mbali na ukweli kuwa kinatumika sana katika duara ya ndani, kiasi cha kuridhisha katika duara ya nje, na kinafundishwa sana katika duara inayopanuka, lugha hii inatumika kuwaunganisha watu kutoka nchi za duara inayopanuka na watumiaji wake wengine. Ingawa lugha hii inadhihirisha udhaifu kidogo katika baadhi ya sifa muhimu za lugha ya kimataifa ni bayana kuwa nafasi yake inaendelea kuimarika na kupata nguvu zaidi. Isitoshe, lugha hii inadhihirisha sifa moja muhimu iliyojadiliwa na Guitu (2010) ya kutumika katika muktadha wa kilimwengu kwa mawasiliano baina ya nchi, na katika muktadha wa ndani kama lugha ya mawasiliano mapana baina ya jamii zenye wingilugha.

### 2.3. Kiswahili Ulimwenguni

Maenezi ya Kiswahili kutoka eneo lake la asili hadi kwingineko Afrika na sehemu mbalimbali za ulimwenguni ni jambo ambalo limejadiliwa na wataalamu wengi, wakiwemo Mazrui & Mazrui (1995), Chimerah (1998), Mulokozi (2004) na Mutiso (2016). Tangu zamani imekuwa ikitumika kwa kiasi fulani katika sehemu za Uarabuni kama vile Omani. Aidha, Kiswahili ni lugha inayozungumzwa na watu wengi katika mataifa mbalimbali ya ulimwengu kama vile Marekani, Uingereza, Ujerumani na kadhalika. Mbali na wazungumzaji wazawa wa Afrika, wapo raia wa nchi hizo mbalimbali za ughaibuni wanaokitumia Kiswahili.

Kiswahili ndiyo lugha yenye asili ya Afrika inayotambulika zaidi nje ya bara la Afrika. Matumizi yake katika matangazo ya redio na kwenye mtandao ulimwenguni yanazipiku lugha zote za Kiafrika Kusini mwa Sahara (Mugane, 2022). Kwa ujumla, upatikanaji wa Kiswahili ughaibuni umechangiwa kwa kiasi kikubwa na asasi mbili muhimu ambazo ni asasi za kielimu pamoja na vyombo vya habari. Kiswahili kinasikika katika matangazo ya mashirika makubwa kama vile VOA, BBC, Radio Deustche Welle, Radio France International, Radio Uchina na Radio Moscow. Kinafundishwa vilevile katika vyuo vikuu vingi sana katika nchi za Marekani, Uingereza, Ujerumani, Upolandi, Meksiko, Uswidi, Uchina na Ubelgiji miongoni mwa nyingine. Hili limekuwa likifanyika katika vyuo maarufu kama vile Harvard, Princeton, Yale, Chuo Kikuu cha London, Bayreuth,

Stanford, Ohio State, Uppsala na Chuo Kikuu cha Masomo ya Kigeni cha Beijing miongoni mwa vyuo vingine .

Kwenye sekta ya filamu, lugha ya Kiswahili imepata fursa kusikika katika filamu kadhaa zilizopata umaarufu kote duniani. Hizi ni pamoja na Star Trek, Out of Africa, The Lion King, na Lara Croft: Tomb Raider. Ingawaje ni maneno machache tu yanayotajwa katika filamu hizi hilo linachangia katika kukitangaza Kiswahili ulimwenguni. Isitoshe, katika The Lion King kuna wahusika wenye majina kama vile Simba na Rafiki, mbali na matumizi ya asante sana na hakuna matata. Nyimbo za wanamuziki mashuhuri kama vile Michael Jackson, Boney M, Miriam Makeba, Franco na kadhalika zimejumuisha lugha ya Kiswahili japo kwa viwango tofauti. Vilevile upanuzi wa matumizi ya mtandao wa intaneti, hasa miongoni mwa vijana, umechangia katika kukikuza Kiswahili. Hili linabainika zaidi tunapozingatia matumizi yake katika mitandao ya kijamii iliyo na wafuasi wengi sana. Aidha, mashirika mashuhuri kama vile Google yametoa nafasi kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Ikumbukwe pia kwamba kamusi tajika ya Oxford imejumuisha maneno kadhaa ya Kiswahili, hatua ambayo inaitangaza zaidi lugha hiyo.

### 2.4. Kiswahili Barani Afrika

Kiswahili ni lugha ya kibantu kutoka Afrika Mashariki. Hata hivyo, ni mojawapo ya lugha muhimu barani Afrika na katika nchi nyingine kama vile katika sehemu za Malawi, jirani na Tanzania, sehemu za Zambia, pamoja na Madagaska (Amidu, 1995). Hizo ni mbali na nchi zilizozoeleka za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Kongo. Anavyoeleza Mugane (2022), wapo watu wengi ambao walichangia maenezi na maendeleo ya Kiswahili kutoka eneo lake la asili hadi kwingineko Afrika na hata nje ya bara hilo. Hawa ni pamoja na: wanasiasa, wapiganiaji wa ukombozi, wasomi watajika, wataalamu wa lugha, wanafasihi na kadhalika. Mifano ni Julius Nyerere, Wole Soyinka, na Ngugi wa Thiong'o. Mathalan, tangu miaka ya 60, Wole Soyinka amekuwa akieleza umuhimu wa kukitumia Kiswahili kama msingi wa kujenga umoja wa Kiafrika. Kilikuwa na uungwaji mkono na makundi mengi ya watu kama lugha mwafaka ya umoja wa Afrika (Amidu,1995).

Chini ya uongozi wa Joachim Chisano, Rais wa zamani wa Msumbiji ambaye wakati huo alikuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, shirika hilo lilikiteua Kiswahili kuwa lugha yake rasmi Julai, 2004. Mugane (2022) anafafanua baadhi ya sababu za hilo kufanyika. Kwanza, Kiswahili kilikuwa kimejijengea sifa kama lugha ya ukombozi, awali katika nchi za Afrika Mashariki lakini baadaye katika nchi za kusini mwa Afrika kwa msaada wa Mwalimu Julius Nyerere wa Tanzania. Pili, Kiswahili kilinasibishwa na mawazo ya kijamaa yanayowajali wanyonge walio wengi. Kwa msingi huo, Uswahili ulinasibishwa na umoja wa aina fulani ambao uligongana na mawazo ya kibepari ya kujilimbikizia mali. Kwa hiyo, ikawa ni rahisi kukikubali.

### 2.5. Kiswahili Afrika Mashariki

Lugha ya Kiswahili ilitekeleza wajibu mkubwa sana katika harakati za kujitakia ukombozi katika nchi za Afrika Mashariki. Kilitumika kama chombo cha kuwaunganisha wananchi, hasa katika nchi za Kenya na Tanzania. Baada ya nchi hizi kupata uhuru, lugha hii iliendelea kushikilia nafasi muhimu kama lugha ya taifa na rasmi nchini Tanzania na kama lugha ya taifa nchini Kenya. Katika mwaka wa 2010, katiba ya Kenya iliitwika lugha hii jukumu la ziada la kuwa lugha rasmi ya kwanza (Constitution of Kenya, 2010). Kiswahili kimekuwa na nafasi muhimu sana pia katika mifumo ya elimu ya mataifa yote matatu ya Afrika Mashariki na baadaye katika nchi jirani za Burundi, Rwanda na Kongo. Aidha, kimetumika katika redio na vyombo vingine vya habari katika nchi zote hizo. Kwa sasa hatua mbalimbali zinachukuliwa ili kiimarike kama lugha ya mawasiliano mapana katika Jumuiya ya Afrika Masahariki. Mulokozi (2004) anataja zifuatazo kama sababu zilizochangia maenezi ya Kiswahili kutoka pwani na kuenea nchini Tanzania na sehemu nyingine za Afrika Mashariki: biashara ya baharini; misafara ya biashara kuingia bara; kuibuka kwa Unguja kama kitovu cha biashara Afrika Mashariki; asili yake ya Kibantu; uislamu; sera ya lugha ya Wakoloni; uchapishaji, vyombo vya habari; siasa, shughuli za wamishionari; sherehe za kitamaduni, mfumo wa elimu na kadhalika.

## 3. Maadhimisho ya Siku Kuu ya Kiswahili

Kongamano Kuu la shirika la Umoja wa Mataifa katika kikao chake cha 41 lilipitisha Azimio 41C/61 lililotambua mchango wa Kiswahili katika kuimarisha utambulisho wa kitamaduni na kuwezesha mawasiliano baina ya wananchi. Kutokana na nafasi ambayo lugha ya Kiswahili imejijengea kwa muda mrefu, kikao hicho kilitangaza tarehe 7 Julai kuwa Siku ya Kiswahili ya Umoja wa taifa na siku hiyo ilisherehekewa kwa mara ya kwanza tarehe 7 Julai, 2022. Uamuzi huo uliidhinishwa rasmi na Mkutano Mkuu wa Shirika hilo mnamo tarehe 2 Julai, 2024. Kufuatia hilo, tarehe 7 Julai itasherehekewa kama Siku ya Kiswahili Ulimwenguni.Tangu Kiswahili kutengewa siku hii, kumekuwa na maadhimisho matatu yaliyoelekezwa na kauli mbiu tofauti. Kutokana na uteuzi wa kuadhimisha Siku ya Kiswahili kote ulimwenguni, shirika la UNESCO linalenga kutambua kuwa:

- Kiswahili ni kati ya lugha za Kiafrika zinazotumiwa zaidi, pia ni lugha ya Kiafrika inayotumiwa zaidi katika Afrika kusini mwa Sahara. Kipo kati ya lugha 10 zinazotumiwa na wasemaji wengi duniani.
- Ni lugha ya mawasiliano (lingua franca) katika nchi nyingi za Afrika ya Kati na Afrika ya Kusini pamoja na Mashariki ya Kati. Kinafundishwa katika vyuo vingi kote duniani.
- Ni lugha rasmi ya Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Isitoshe, Tarehe 7 Julai ilichaguliwa kukumbuka:

- Tarehe 7 Julai, 1954 ambako chama cha TANU chini ya uongozi wa mwalimu Julius Nyerere kiliamua kutumia Kiswahili kwa ajili ya shughuli zake za kupigania uhuru wa Tanganyika.

- Tarehe 7 Julai, 2000 ambako mkataba juu ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki iliyofufuliwa ulipata kuwa rasmi. Jumuiya hiyo iliunganisha nchi za Tanzania, Kenya na Uganda zenye wasemaji wengi wa Kiswahili.

Hatua hii imetokana na juhudi za wataalamu na wapenzi wengi wa Kiswahili ambao wamechangia kwa kukitangaza na kukipa hadhi. Je nini nafasi ya wadau hawa katika kuiweka Kiswahili kwenye nafasi yake ulimwenguni?

### 3.1. Shughuli za Wizara

Maadhimisho ya tatu ya Siku kuu ya Kiswahili yaliyofanyika nchini Kenya yalihusisha wizara ya Jinsia, Utamaduni, Sanaa na Turathi. Kwa mujibu wa Ontieri (2017) Kenya kama nchi iliyo na ukwasi mkubwa wa kimatumizi ya Kiswahili barani Afrika ina nafasi ya kipekee ya kueneza na kukuza Kiswahili Barani na Ulimwenguni kote. Mojawapo ya majukumu ya kimsingi ya wizara hii ni kuendeleza matumizi ya Kiswahili, lugha ya ishara na lugha nyingine asilia (Executive order No.2, 2023). Mnamo mwaka wa 2024, aliyekuwa Waziri katika wizara hii Bi. Aisha Jumwa alibuni kamati andalizi ya wanajopo 17 kuweka mipango mwafaka ya maadhimisho ya siku hii. Idadi kubwa ya wanakamati walitoka katika Idara mbalimbali za serikali na hivyo kuwa na uwakilishi mchache sana wa wadau wengine. Awali, KAKAMA ilipanga kuwa Rwanda iwe mwenyeji lakini nchi hiyo haikuwa tayari. Kutokana na hali hiyo, Kenya iliombwa kuwa mwenyeji wa sherehe hiyo. Nchi ya Kenya ilichelewa kukubali ombi hilo, hivyo kucheleweshа matayarisho na mipango iliyohitajika. Hata hivyo, hatimaye serikali ya Kenya ilifadhili bajeti kwa kiasi kikubwa cha hela. Kulitolewa tetesi kwamba KAKAMA haikutimiza wajibu wake kwa muda licha ya ukweli kwamba ilistahili kufadhili sehemu ya bajeti ya shughuli hiyo. Kulingana na mmoja wa wanakamati waliohojiwa, utaratibu wa mawasiliano kati ya KAKAMA na waandalizi nchini Kenya haukuwa mzuri, hali ambayo iliathiri shughuli nzima. Pili, Kamisheni ina wafanyikazi wachache sana jambo ambalo lilitinga uwezo wao wa kutimiza majukumu yote kikamilifu kwa kushirikiana na wizara. Tatizo lingine lilikuwa kuchelewa kutoa barua za mialiko kwa wajumbe kutoka sekta mbalimbali. Hali hii ilipelekea wajumbe wengi kukosa kuhudhuria jambo lililodhihirika kutokana na barua nyingi za mwaliko zilizosalia kwenye meza ya usajili. Kulingana na mmoja wa washiriki, baadhi ya walioalikwa na wizara katika kongamano hawakutoa mchango wowote kuhusu mijadala iliyokuwepo. Huenda hawakufamishwa wajibu wao kwenye Kongamano hilo ama hawakuwa na uelewa mzuri wa maswala yaliyopaswa kuzingatiwa. Mwanakamati mwingine alidai kuwa wataalamu kutoka nchi wanachama hawakuteuliwa vizuri kwani wataalamu wa Kiswahili walikuwa wachache na hivyo kuathiri uwakilishi uliotarajiwa. Mwisho, ufadhili uliotolewa na serikali kupitia wizara haukuwafikia wajumbe wengine waliosikika wakilalamikia kutofadhiliwa.

Makala hii inapendekeza kusuluhishwa kwa changamoto kama hizi ili kuimarisha maadhimisho yajayo katika nchi zitakozoteuliwa kuandaa sherehe za maadhimisho. Inapendekeza mipango ya mapema, ratiba na mialiko ya mapema, uhusishaji wa wadau wote haswa wanataaluma na ufadhili wa wajumbe wote wanaowakilisha taasisi muhimu vikiwemo vyama vya kitaaluma na vyuo vikuu. Ushirikiano wa namna hii, unaosisitizwa na Deutsch & Krauss (1962) ndio utafanikisha maadhimisho katika siku za usoni.

### 3.2. Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA)

Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA) ina jukumu la kuratibu na kukuza maendeleo na matumizi ya Kiswahili katika kanda nzima na kwingineko. Ina jukumu la kuhakikisha maendeleo ya Kiswahili kama lingua franka kwa mwingiliano wa kikanda na kimataifa kwa maendeleo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kitamaduni, kielimu, kisayansi na kiufundi. KAKAMA inatimiza wajibu wake kupitia utafiti, ufundishaji, ujifunzaji na ukuzaji wa Kiswahili kupitia uundaji wa sera, uzalishaji wa maarifa na uhakiki wa mitaala na kusanifisha istilahi. KAKAMA ndiyo taasisi kuu ya ushauri ya Jumuiya kuhusu masuala yote yanayohusiana na Kiswahili (Simala, 2019).

Kamisheni ina wajibu wa kushirikiana na vyama vya Kiswahili, taasisi mbalimbali na wizara mbalimbali katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili (Simala, 2019). Hili linaoana vizuri na mapendekezo ya Deutsch (1949) kuhusu umuhimu wa ushirikiano. Maadhimisho ya siku kuu ya Kiswahili ni sehemu muhimu sana ya shughuli ambazo Kamisheni ya Kiswahili inapaswa kuzitekeleza.

### 3.3. Kongamano la KAKAMA

Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA) huandaa kongamano sambamba na sherehe za Siku kuu ya Kiswahili. Mojawapo za hatua za maandalizi ya kongamano ni kutoa tangazo la wito wa makala na baadaye kuamua ni makala yapi yatakayowasilishwa. Mialiko hutolewa na KAKAMA na wizara husika katika nchi inayoandaa maadhimisho. Makongamano ya KAKAMA ni njia moja ya kuleta pamoja wadau wa Kiswahili kama vile wahadhiri wa Kiswahili, watafiti, wanafunzi miongoni mwa wengine. Ni katika makongamano kama haya ambapo waliofika katika kongamano huhusishwa kwa kutoa nafasi ya kuwasilisha makala kupitia majopo na kushiriki katika mijadala inayoibuka.

Kongamano la mwaka 2024 liliratibiwa kufanyika siku ya kwanza ya maadhimisho. Shughuli kuu ya Kongamano ikiwa mawasilisho ya kitaaluma kwa kurejelea Kauli Mbiu, "Elimu na Wingi Lugha katika Ufanikishaji wa Amani". Kulingana na mmoja wa wanakamati aliyehojiwa, kongamano lilifanikiwa kwa kiasi kidogo sana kwa sababu kadhaa. Kwanza, waalikwa wengi hawakuhudhuria. Ikisiri zilizotumwa zilikuwa 32 ambayo ni idadi ndogo sana ikilinganishwa na idadi ya wataalamu walioko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAM) kwani ndicho kitovu cha wasemaji na wataalamu wa Kiswahili. Kati ya ikisiri 32 zilizopokelewa, wajumbe 20 pekee walifika. Hali hii inahusishwa na sababu anuwai kama vile: Tatizo la mawasiliano, KAKAMA kufanya shughuli zote na kutowahusisha wadau wengine, Kenya kama nchi mwenyeji kuchelewa kukubali wito wa kuwa

mwenyeji na hivyo kuchelewesha harakati ya kutangaza wito wa Makala. Kulingana na nadharia ya Ushirikiano ya Deutsch (1949), kungefanyika mawasiliano mapema na kisha kuwashawishi wajumbe kuhudhuria kongamano kwani watu katika ushirikiano huelewana na kuathiriana kimawazo (Crombag, 1966; Deutsch,1949; Deutsch & Krauss,1962). Ushirikiano pia ungehimiza kutafuta na kutoa taarifa kuhusu kazi za shirika kama wanavyoeleza Zander & Wolf (1964). Kwa kufanya hivyo taarifa ingewafikia wadau wote kwa wakati unaofaa na kutatua tatizo la mawasiliano.

### 3.4. Jamii na Utamaduni wa Waswahili

Utamaduni ni jumla ya matendo, fikra, mifumo ya maisha na viashiria vyote vinavyoweza kumwongoza na kumtambulisha mtu (Ponera, 2014). Pia, ni mkusanyiko wa mila na desturi zote za jamii inayotumia lugha mahsusi (Newmark, 1988). Swala la Waswahili na utamaduni wa Waswahili lilibainika kwa uzito katika hotuba za "Usiku wa Mswahili", madai yakiwa kwamba, Kiswahili ni lugha iliyo na wenyewe. Kwamba lugha hufungamana na utamaduni na hivyo ulimwengu ukichukua Kiswahili, uchukue pia utamaduni wake. Dhana ya Mswahili imeelezwa na wataalam mbalimbali. Kwa wataalam wa Kiswahili, Uswahili ni zaidi ya maeneo ya kuishi, ni ustaarabu katika nyanja zote. Katika hotuba yake, Profesa Rayya Timammy aligusia suala hili na kuainisha Waswahili katika makundi matatu: Mswahili asilia, Mswahili msemaji na Mswahili mwanataaluma. Shughuli ya Maadhimisho ya Sikukuu ya Kiswahili 2024 ilifikia kilele chake usiku wa Jumamosi ambapo paliandaliwa sherehe ya Usiku wa Mswahili zilizodhamiriwa kusawiri utamaduni kamili wa Mswahili. Walioazimia kuhudhuria walitakiwa kuvaa mavazi ya Waswahili. Matukio ya usiku yalijumuisha muziku wa taarabu, ngoma na vyakula vya Waswahili. Washiriki wote walikaribishwa kwenye sherehe kwa madafu. Nene (2018) katika BBC Swahili anamnukuu msemaji mmoja aliyeeleza kuwa, "Madafu ni zao kubwa ambalo tunategemea sisi Wapwani, halafu haya madafu ni tiba kubwa sana…". Kama lugha ya ulimwengu ni vyema kukipa Kiswahili mwelekeo faafu wa maadhimisho utakaokipaisha Kiswahili katika ngazi yake inayostahiki kwa kuhusisha matukio yasiyofungamana na jamii moja.

Kauli ya kijumla hata hivyo ilikuwa kwamba Kiswahili ni cha Waswahili asilia wenye lugha na utamaduni wao. Kwa hivyo, ulimwengu unapochukua Kiswahili, uchukue na utamaduni wake. Je mtazamo huu ukiendelezwa utaifaa lugha ya Kiswahili kama lugha ya ulimwengu au la? Katika maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani basi Kiswahili ni cha nani? Maadhimisho ya siku hii basi yasilenge kusawiri jamii moja kama wenye kumiliki lugha ya Kiswahili. Yalenge makundi yote yanayotumia lugha hii katika ngazi na miktadha mbalimbali. Hawa ni wasemaji, wataalamu na Waswahili wazawa. Ni katika msingi huu ambapo Kiswahili kilisanifishwa ili kikubalike na kutumika kama lugha rasmi na ya ulimwengu. Hans (2017) analipigia suala la usanifishaji upya wa Kiswahili debe ili kurahisisha matumizi yake katika Jumuiya ya Afrika mashariki na ulimwengu mzima.Kiswahili hakiwezi kufungiwa katika eneo maalum kwani hali hii inaweza kusababisha ushindani na ubinafsi. Ushindani husababisha kudidimiza malengo, uchokozi, uadui, uzuizi na ukosefu wa ushawishi (Rocha & Rodgers, 1976; Tjosvold, 1983).

Lugha na utamaduni havipaswi kuunganishwa kuwa kitu kimoja kwa sababu lugha moja inaweza kubeba utamaduni tofauti Kwa mfano lugha za kundi la Kihindi la Kihindi-Kiulaya za Kingereza, Kifaransa na Kihindi ambazo ni lugha za kimataifa zinazozungumzwa na jamii mbalimbali zenye tamaduni anuwai. Crystal (2003) na Crystal (2006) wakizungumzia nini kinachofanya lugha kuwa ya ulimwengu, anataja mambo mawili makuu kuwa uwezo wa kisiasa na kiuchumi. Lugha za Kigirki, Kilatini, Kiarabu, Kihispania, Kibelgiji na Kifaransa zilikua kutokana na uwezo wa Kisiasa. Kiswahili kimefikia kiwango hiki na hivyo sherehe za maadhimisho yake zinastahili kulenga kuijenga kama lugha ya ulimwengu na si kama lugha inayohusishwa na jamii na utamaduni mmoja. Mwasaru (2023) anasema kuwa lugha ni kitu hai kinachobadilika na kadri lugha inavyobadilika ndivyo utamaduni pia unafaa kubadilika. Lugha ya Kiswahili sanifu imepitia mabadiliko mengi. Iwapo basi itafungamanishwa na utamaduni wa wasemaji wake haiwezi kufungiwa kwenye utamaduni wa Waswahili wa Mwambao wa Kenya. Kwa kuzingatia maoni ya Crystal (2003) na Crystal (2006) ni muhimu kuimarisha hali yetu ya kiuchumi ili kukisukuma mbele Kiswahili. Mambo ya kutiliwa mkazo ni kukuza njia za kisasa na matumizi yake katika nyanja za sayansi, teknolojia na mawasiliano, kukuza mashirika, viwanda na biashara, vyombo vya habari, sanaa na kukuza viwango vya kiakademia na utafiti kuhusu lugha ya Kiswahili.

### 3.5. Maadhimisho katika Vyuo Mbalimbali

Maadhimisho ya Siku kuu ya Kiswahili duniani hufanyika kwa njia mbalimbali kote duniani. Maadhimisho ya 2024 yalithibitisha ufanisi mkubwa wa lugha ya Kiswahili. Ufanisi huu unajumuisha kutimiza lengo la 17 la malengo endelevu (Sustainable Development Goals, 2018) kuhusu kuwepo kwa ushirikiano katika kufanikisha malengo hayo, hili linaashiria ushirikiano wa wadau wote katika ukuzaji na matumizi ya Kiswahili. Akitoa maoni yake, kuhusu malengo ya maadhimisho ya Kiswahili Mutiso (2016) anahimiza matumizi na ukuzaji wa lugha nzuri na tajiri kwa namna inayosaidia kujenga umoja na kukuza uelewa wa pamoja.

Vyuo vikuu mbalimbali vilifanya mipango ya kusheherekea Siku kuu ya Kiswahili kwa njia tofauti ingawa vichache vilifanikiwa. Mwaka 2022, Chuo kikuu cha Kibabii kiliandaa sherehe hizi; Chuo Kikuu cha Maseno kwa kushirikiana na Kundi la Wanahabari kutoka Nation walipanga sherehe ya 2024 ambayo haikufua dafu. Baadhi ya wataalamu walikosa kuhudhuria sherehe hizi kwa kukosa mipango mwafaka na hivyo kuacha pengo lisiloweza kuzibwa na taasisi nyinginezo. Kwa mfano, kati ya idadi kubwa ya Maprofesa wa Kiswahili nchini Kenya Wanne tu ndio waliohudhuria maadhimisho yaliyoandaliwa Mombasa. Vilevile idadi ya wahadhiri na wadau walioalikwa ilikuwa ndogo kuliko ilivyotarajiwa. Vyuo vikuu kwa kuwa taasisi za kitaaluma zinazotoa

mchango mkubwa kwa ukuzaji wa Kiswahili kwa njia za kiusomi zinastahili kuwa katika mstari wa mbele katika maadhimisho haya. Ni lazima kuhimiza ushirikiano wa wadau ambao utawezesha kuwasilana kuhusu kazi, kusaidiana na kugawana kazi (Deutsch, 1949; Thomas 1957; Zander & Wolf, 1964). Kama anavyoeleza Ontieri (2017), vyuo vikuu vina nafasi muhimu kwa maendeleo yoyote yale kwani ni taasisi za maarifa zinazojumuisha wahadhiri, watafiti na wanafunzi. Ufanikishaji wa Kiswahili kwa viwango vya kiulimwengu hivyo utahitaji mchango mkubwa wa wataalamu kutoka vyuo vikuu hususan katika awamu hii ya pili ya usanifishaji upya wa Kiswahili.

## 4. Hitimisho na Mapendekezo

### 4.1. Mapendekezo

Kutokana na mjadala kwenye makala hii mapendekezo kadhaa yametolewa. Kwanza, mipango ya maadhimisho ya Siku kuu ya Kiswahili ianzishwe mapema katika nchi mwenyeji na wizara yake. Hii ni pamoja na uteuzi na makubaliano ya mapema kuhusu nchi mwenyeji. Nchi hiyo iridhie kwa wakati na KAKAMA iingie kwenye mchakato wa kuratibu shughuli hiyo mapema. Pili, KAKAMA na wizara husika zihusishe wadau wote muhimu katika swala zima la Kiswahili kutoka sekta mbalimbali zinazohusika. Kuwashirikisha wadau mbalimbali kutapanua wigo wa washirika, kusaidia katika usambazaji wa habari kuhusu shughuli hiyo na kuwafanya wengi kuhisi kuwa hili ni jambo la wote.

Tatu, changamoto zilizobainika katika maadhimisho yaliyopita zichukuliwe kama uzoefu wa kuchangia maandalizi ya sherehe bora. Zifanyiwe tafakari ya kina na kutafutiwa ufumbuzi kabla ya maadhimisho yajayo katika mataifa yatakayoteuliwa. Inapendekezwa mipango ya mapema, ratiba na mialiko ya mapema, uhusishaji wa wadau wote haswa wanataaluma na ufadhili wa wajumbe wote wanaowakilisha taasisi muhimu vikiwemo vyama vya kitaaluma na vyuo vikuu.

Nne, ingawa kuna ukuruba mkubwa kati ya lugha na utamaduni wa jamii inayoizungumza, maadhimisho ya siku kuu ya Kiswahili duniani yatenganishwe na utamaduni wa jamii maalum. Utamaduni wa Waswahili utambuliwe kwa sababu ni wa msingi katika ukuzaji wa lugha hiyo lakini maadhimisho yasilenge kusawiri jamii moja kama yenye kumiliki lugha ya Kiswahili. Yahusishe makundi yote yanayotumia Kiswahili katika ngazi na miktadha mbalimbali kwani hivi sasa Kiswahili ni lugha ya ulimwengu. Hawa ni wasemaji, wataalamu na Waswahili wazawa.

Tano, vyuo vikuu kama taasisi za kitaaluma zinazotoa mchango mkubwa kwa ukuzaji wa Kiswahili kwa njia za kiusomi, ziwekwe katika mstari wa mbele katika maadhimisho haya. Hata hivyo, ingawa ni vyema kuwa na sherehe moja kubwa katika ngazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni muhimu tukubali kuwa haiwezekani wahusika wote kushiriki. Kwa sababu hiyo, sherehe nyingine zifanyike katika vyuo mbalimbali lakini kwa kuhusisha vyuo kadhaa katika maeneo maalum ili kuhakikisha kuwa vyuo na taasisi zote zinazoshughulikia lugha ya Kiswahili zimepata fursa.

Hatimaye, uongozi wa vyama vya Kiswahili kama CHAKITA, CHAKAMA, CHAUKIDU na CHALUFAKITA uhusishwe ili kutoa ushauri kwa wanachama wao kushirika maadhimisho ya siku zijazo. Vyama hivi tayari vina njia maalumu za kuwasiliana na wanachama wao na vitasadia sana katika kuhakikisha kuwa taarifa zinawafikia na sherehe za maadhimisho katika sehemu mbalimbali zinafana.

### 4.2. Hitimisho

Makala hii inahitimisha kuwa lugha ya Kiswahili ina nafasi muhimu sana katika jamii kimataifa na katika ngazi ya ulimwengu. Imefikia kiwango cha lugha za ulimwengu na hivyo inastahili kupewa msukumo kwa kutumia mikakati itakayoiwezesha kuafiki nafasi hiyo. Tangu zamani, lugha hii imetekeleza majukumu muhimu katika jamii, hasa katika kitovu chake cha Afrika Mashariki. Nafasi yake imeendelea kuboreka kadri ya mpito wa wakati na upanuzi wa maeneo inamotumika. Isitoshe, asasi mbalimbali muhimu katika ngazi ya kikanda na barani Afrika zimeendelea kuitambua, hali ambayo inaipa hadhi zaidi. Kilele kilikuwa uamuzi wa shirika la Umoja wa Mataifa kuitengea siku maalum ya kuishereheka. Katika muktadha huo, maadhimisho ya siku hiyo yanapaswa kushughulikiwa kwa makini kama njia ya kudhihirishia ulimwengu kwamba lugha hii ilistahili nafasi hiyo. Makala inapendekeza kuwa mipango ya maandalizi ya maadhimisho hayo itiliwe maanani na wahusika wote ili kuhakikisha kuwa inafanikiwa. Aidha, swala la ushirikiano kati ya wadau mbalimbali lipate kipaumbele katika siku za usoni.

### Marejeleo


Amidu, A. A. (1995). Kiswahili, a Continental Language: How Possible Is It? (Part I), Nordic Journal of African Studies 4(2): 50-70 (1995).

Chimerah, R. M., (1998). Kiswahili: Past, Present and Future Horizons. Nairobi: Nairobi University Press.

Crombag, H. F. (1966) Cooperation and Competition in Meeams Interdependent Triads. Journal of Personality & Social Psychology. Vol.4 (pp.692-695).

Crystal, D. (2003). English as a global Language. UK: University of Cambridge Press http://www.Cambridge.org ilipakuliwa 1-10-2024

Crystal, D. (2006). English worldwide. In, R. Hogg & D. Denison (Eds.), A history of the English language (pp. 420-444). Cambridge: Cambridge University Press.

Dewi, A. (2012). English as an International Language: An Overview. Journal of English and Education, Vol. 6 No.2 - December 2012.

Deustsch, M. (1949). An Experimental Study of the effects of Cooperation and Competition upon group process. Human Relations, Vol. 2 (pp.199-231).

Deustsch, M. &Krauss, R. M. (1962). Studies in Interpersonal Bargaining Journal of Conflict Resolution-

Executive order NO.2 (2023) Organisation of the republic of Kenya. Issued by the Executive office of the President. https://www.president.go.ke

Guitu, T. (2010). Features of an International Language. Ştiinţe socioumane, ediţia a X-a.

Hans, M. M. (2017). Usanifishaji wa Kiswahili Afrika Mashariki: Changamoto na namna ya kukabiliano nazo. JULACE: Journal of University of Namibia Language Centre. Vol. 2.No.2 2017

Kachru, B. (1985). Standards, codification and sociolinguistic realism: The English language in the outer circle. In, R. Quirk & H. Widdowson (Eds.), English in the World: Teaching and Learning the Language and Literatures (pp. 11-30). Cambridge: Cambridge University Press.

Mazrui,A & Mazrui,A(1995) Swahili, State and Society. The political economy of an African Language: East African Educational Publishers https://api.semanticsscholar.org/corpus ID:141543398

Mugane, J. (2022). The story of how Swahili became Africa's most spoken language, https://theconversation.com/kiswahili-how-a-standard-version-of-the-east-african- language-was-formed-and-spread-across-the-world-208251

Mulokozi, M. M. (2004). Kiswahili as a National and International Language, H Net; Humanities and Social Sciences Online: Department of History, 1995 – 2006.

Mutiso, K. (2016). Mapisi, Kuenea na Ufundishaji wa Kiswahili Duniani. Katika, Leonard, M. Chacha (mh.). Kiswahili na Utandawazi. Nairobi: Twaweza Publications. Kur. 68-92.

Mwasaru, B.(2023). Lugha na Utamaduni. Mozilla foundation. https://foundation.mozilla.org

NewMark, M. (1988). The Translation Procedures of Cultural Expressions Applied in a game of Thrones

Nene, J. (2018), BBC Swahili https://www.bbc.com ilipakuliwa 6/8/24

Okombo, P. L. & Muna, E. (2017). The International Status of Kiswahili: The Parameters of Braj Kachru's Model of World Englishes. Africology: The Journal of Pan African Studies, vol. 10, no.7.

Ontieri, J.(2017). Nafasi ya Kiswahili kama lugha rasmi nchini Kenya. Katika, Lugha na Fasihi katika Karne ya 21. Eldoret: Moi University

Ponera, A.S. (2014).Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi. Dar es Salam, Karljamer Print Technology.

Rocha, A & R. W (1976) Aves &Babbit in the classroom: Effects of Competition and reward on childrens aggression. Journa of Personality and Social Psychology

Simala, K.I. (2019). Mitaala ya Kiswahili katika Vyuo vya Afrika Mashariki. Zanzibar. KAKAMA.

Smith, L. E. (1976). English as an International Auxiliary Language. RELC Journal, 7(2), 38-42. https://doi.org/10.1177/003368827600700205

The Constitution of Kenya (2010). National Council for how Reporting. Lof Kenya: Nairobi. http://www.parliament.go.ke

Thomas (1957). Effects of facilitative role interdependence on group functioning. Human Relations (347-366)

Tjosvold, D (1984). Cooperative Theory and Organisations. Human Relations 37(9) 743-767 DOI: 1177/001872678403700903

UNESCO, (2021). Kiswahili Day. General Conference, 41st Session, Paris, 2021 41 C/61 5 November 2021.

Zander A. &Wolf, D. (1964). Administrative Rewards and Coordination among Committee Members. Administrative Science Quaterly Vol.9:50-59.